KISWAHILI LUGHA KAZI YA DISEMBA — GRADE 3

Jina la Mwanafunzi: _____

Nambari ya Mtihani: _____

Darasa / Mkondo: _____

Tarehe: _____

Sahihi: _____

SEHEMU A: KUSOMA, KUSIKILIZA NA KUONGEA

1. Kusoma kwa Sauti

Soma kifungu hiki kwa sauti kwa kuzingatia matamshi, kasi, sauti na alama za uandishi.

Katika dunia kuna ndege wa aina mbalimbali. Ndege ninayempenda zaidi anaitwa Kasuku. Kasuku huiga sauti za watu na ndege wengine. Kasuku alisherehekea sikukuu ya kuzaliwa kwake mwezi uliopita. Aliwaalika ndege wengine kama kuku, bata, horeo, kanga na batamzinga.

Mwalimu atathmini ufasaha wa mwanafunzi.

2. Kusikiliza na Kuongea

Mwalimu asome kifungu hiki kwa sauti kisha awaulize wanafunzi maswali yafuatayo.

Huu ni mti mkubwa sana. Ni mti wa maembe. Hamisi amevuna maembe kumi. Anayaweka kwenye kikapu cheusi.

Maswali

a) Mti huu ni wa aina gani?

---

b) Nani amevuna maembe?

---

c) Hamisi amevuna maembe mangapi?
